
NISHATI
HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati.go.tz Wizara ya Nishati wizara_ya_nishati_tanzania @Nishati2017 Wizara ya Nishati
Toleo Namba 23 Februari 1 - 28, 2021

# WAZIRI KALEMANI AIAGIZA TPDC KUKAMILISHA UFUNGAJI WA MITAMBO YA KUSINDIKA GESI ASILIA KWA MATUMIZI YA MAGARI NDANI YA MIEZI SITA



# NAIBU WAZIRI BYABATO AITAKA TANESCO ISHIRIKIANE NA MBUNIFU WA MTAMBO WA KUFUA UMEME KWA KUTUMIA SUMAKU KUTENGENEZA MTAMBO MWINGINE MPYA



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

# WAZIRI KALEMANI AIAGIZA TPDC KUKAMILISHA UFUNGAJI WA MITAMBO YA KUSINDIKA GESI ASILIA KWA MATUMIZI YA MAGARI NDANI YA MIEZI SITA

**Na Dorina Makaya – Dar-es-salaam.**

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kusindika Gesi Asilia (Compressed Natural Gas - CNG) kwa matumizi ya magari ndani ya miezi sita.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani mara baada ya kuwasili kwenye eneo la mradi wa usindikaji wa Gesi Asilia (Compressed Natural Gas-CNG) itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – DART) katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari yaendayo kasi cha DART kilichopo Ubungo jijini Dar-es-salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Dar-es-Salaam, tarehe 23 Januari, 2021 kwa ajili ya kujionea maendeleo ya Mradi wa DART unaotarajiwa kutumia gesi asilia (CNG) itakayosambazwa na TPDC.

Waziri Kalemani ametoa maagizo hayo kwa TPDC tarehe 23 Januari, 2021 wakati alipotembelea eneo linalojengwa mradi wa usindikaji  Gesi Asilia iliyokandamizwa (Compressed Natural Gas-CNG) itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – DART) katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari yaendayo kasi cha DART kilichopo Ubungo jijini Dar-es-Salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani katika jiji la Dar-es-salaam.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akipata maelezo ya maendeleo ya mradi kutoka kwa Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta  wa TPDC, Dkt. Wellington Hudson wakati  alipotembelea mradi wa Usindikaji wa Gesi Asilia (Compressed Natural Gas-CNG) itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – DART) katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari yaendayo kasi cha DART kilichopo Ubungo jijini Dar-es-Salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Dar-es-salaam tarehe 23 Januari, 2021.

Waziri Kalemani ameiagiza TPDC kutoa

# WAZIRI KALEMANI AIAGIZA TPDC KUKAMILISHA UFUNGAJI WA MITAMBO YA KUSINDIKA GESI ASILIA KWA MATUMIZI YA MAGARI NDANI YA MIEZI SITA




Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari wakati alipotembelea Mradi wa Usindikaji wa Gesi Asilia (Compressed Natural Gas-CNG) itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – DART) katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari yaendayo kasi cha DART kilichopo Ubungo jijini Dar-es-salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Dar-es-Salaam tarehe 23 Januari, 2021.

huduma hiyo si tu kwa magari 300 yaendayo kasi, bali pia kwa watumiaji binafsi ili kuongeza kipato kwa Serikali,  kuipunguzia DART gharama za uendeshaji na hivyo kuleta unafuu wa gharama za nauli ya mabasi kwa wananchi.

"Sitakuja kuzindua matumizi ya Gesi Asilia kwa magari 300 tu. Ongezeni wigo wa watumiaji wa gesi asilia kwa magari mengine yakiwemo ya watu binafsi." Amesema Dkt. Kalemani

Aidha, Waziri huyo wa Nishati, ameongeza kuwa, matumizi ya gesi asilia kwenye magari ya watu binafsi yataleta unafuu mkubwa wa gharama ikilingalishwa na matumizi ya Petroli na dizeli kwa zaidi ya asilimia 45.

Vilevile, Waziri Kalemani amewashauri wananchi kufunga mfumo utakaowawezesha kutumia gesi asilia kwenye magari yao ambao utawapa unafuu mkubwa katika matumizi ya magari yao.

Dkt. Kalemani amesema, kwa sasa kuna magari takriban 800 yanayotumia gesi, hivyo amewashauri wananchi wenye magari na vyombo vingine vya moto waongeze mfumo utakaowawezesha kutumia gesi asilia, na kwamba, huduma hiyo ya kufunga mfumo kwa ajili ya kutumia gesi asilia inapatikana katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaaam na Taasisi ya Teknolojia ya Dar-es-Salaam (DIT).

Waziri Kalemani amesema, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Akifafanua zaidi kuhusu mradi huo Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. Mataragio amebainisha kuwa, TPDC imepanga kujenga vituo vitano vya CNG ambapo kati ya hivyo, viwili vitakuwa vituo vikuu (CNG mother stations) na vitatu vitakuwa vituo vidogo (CNG daughter Stations) ambapo Kituo Kikuu kimoja kitajengwa eneo la Ubungo linalomilikiwa na DART maalum kwa

# WAZIRI KALEMANI AIAGIZA TPDC KUKAMILISHA UFUNGAJI WA MITAMBO YA KUSINDIKA GESI ASILIA KWA MATUMIZI YA MAGARI NDANI YA MIEZI SITA




Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari wakati alipotembelea mradi wa Usindikaji wa Gesi asilia (Compressed Natural Gas-CNG) itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi (Dar es Salaam Bus Rapid Transit – DART) katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari yaendayo kasi cha DART kilichopo Ubungo jijini Dar-es-salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Dar-es-salaam tarehe 23 Januari, 2021. Kushoto kwa Waziri Kalemani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio.

mabasi ya mradi wa BRT uliozoeleka kama mwendokasi ambapo kitakuwa na uwezo wa kujaza gesi katika mabasi zadi ya 300 kwa siku.

Aidha, ameeleza kuwa, kituo Kikuu cha pili kitajengwa pembezoni mwa barabara ya Sam Nujoma katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambapo kituo hiki kwa kuanzia kitakuwa na uwezo wa kujaza gesi katika magari zaidi ya 200 kwa siku na pia kitatumika kuhudumia vituo vidogo (CNG daughter stations) vitakavyojengwa katika maeneo mbalimbali.

Akizungumzia ujenzi wa vituo vidogo, Dkt. Mataragio amesema, vituo hivyo vitajengwa eneo la Soko kuu la samaki Feri, Hospitali ya Muhimbili, pamoja na Galagaza-Kibaha katika eneo la ukanda wa viwanda.

Amesema, Kituo cha Soko Kuu la samaki Feri kitakuwa na uwezo wa kujaza gesi katika magari zaidi ya 200 kwa siku.

Dkt. James Mataragio, amemuahidi Waziri Kalemani kuwa, atahakikisha wanatekeleza maagizo yote aliyowapatia.

# NAIBU WAZIRI BYABATO AITAKA TANESCO ISHIRIKIANE NA MBUNIFU WA MTAMBO WA KUFUA UMEME KWA KUTUMIA SUMAKU KUTENGENEZA MTAMBO MWINGINE MPYA

**Na Dorina Makaya – Dar-es-salaam.**

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kushirikiana na Mbunifu wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku, kutengeneza mtambo mwingine mpya ndani ya wiki mbili.

Naibu Waziri Byabato ametoa maelekezo hayo, tarehe 25 Januari, 2021 alipomtembelea mbunifu huyo, Bw. Rojers Msuya (52) nyumbani kwake Kawe, jijini Dar-es-salaam kushuhudia ubunifu wake wa kutengeneza mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku baada ya kupata taarifa kuhusiana na mbunifu huyo.

Naibu Waziri Byabato amesema, gharama zote za kutengeneza Mtambo huo, zitagharamiwa na Serikali kupitia shirika lake la TANESCO. Aidha, ameeleza kufurahishwa kwake na ubunifu huo, na kusema kuwa kufanikiwa kutengeneza mtambo wenye uwezo mkubwa wa kufua umeme kwa kutumia sumaku kutawezesha maeneo ambayo bado hayajafikiwa na umeme wa TANESCO na REA kupata umeme kwa gharama nafuu.




Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato (kushoto) akizungumza na Mbunifu wa Mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku Bw. Rojers Msuya (52) Mkazi wa Kawe, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar-es-salaam. Mtambo unaoonekana hapo chini katika picha una uwezo wa kuzalisha umeme KVA 5 sawa na WATT 5000.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato (katikati) akisoma kipimo cha umeme kinachotumika kupima kiwango cha umeme kinachozalishwa kwenye mtambo wa kufua umeme kinachoitwa (Clamp digital meter) kipimo hicho kimethibitisha kuwa, umeme unaozalishwa na mtambo uliobuniwa na Mbunifu Rojers Msuya (kulia), unakidhi viwango vyote vya TANESCO.

Naibu Waziri Byabato amemhakikishia Bw. Rojers Msuya kuwa, teknolojia ya kutengeneza mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku ikifanikiwa, atahakikisha Haki miliki zake zote kuhusiana na ugunduzi huo zinalindwa na kuhakikisha kunakuwepo

# NAIBU WAZIRI BYABATO AITAKA TANESCO ISHIRIKIANE NA MBUNIFU WA MTAMBO WA KUFUA UMEME KWA KUTUMIA SUMAKU KUTENGENEZA MTAMBO MWINGINE MPYA



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Umeme wa Wizara ya Nishati, Mha. Innocent Luoga (kushoto), kabla ya kukutana na Mbunifu wa ufuaji umeme kwa kutumia sumaku. Aliye kati ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji - Usafirishaji wa TANESCO Mha. Isaac Chanji (akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO)




Rojers Msuya (52), Mkazi wa Kawe, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar-es-salaam (kulia), ambaye ni Mbunifu wa Mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku akizungumza na waandishi wa habari, tarehe 25 Januari, 2021 nyumbani kwake Kawe jijini Dar-es- salaam mara baada ya Kutembelewa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato (kushoto).

na mikataba ya kisheria katika kushirikiana na TANESCO katika kutengeneza mitambo hiyo.

Naye Mbunifu huyo wa Mtambo wa kufua umeme kwa kutumia sumaku, Bw. Rojers Msuya, amemweleza Naibu Waziri Byabato kuwa, mtambo alioutengeneza una uwezo wa kuzalisha KVA 5 sawa na WATT 5000 na kuwa endapo atapata ushirikiano kutoka serikalini ataweza kupanua teknolojia hiyo aliyoibuni ya kufua umeme kwa kutumia sumaku.

Bw. Rojers amemweleza Naibu Waziri Byabato kuwa, hadi sasa, tayari amekwishatengeneza mashine 10 za majaribio za kufua umeme kwa njia ya sumaku na kuwapatia watu mbali mbali kuifanyia majaribio mitambo hiyo na hakuwahi kupata malalamiko yoyote kutoka kwa watumiaji hao kwa kipindi cha miaka minane sasa.

Bw. Rojers amesema sifa za Mitambo hiyo aliyoibuni ni kuwa haina kelele, haichafui mazingira na inaweza kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 bila ya kufanyiwa matengenezo.

Vilevile, Bw. Rojers amemshukuru Naibu Waziri Byabato pamoja na viongozi wengine wa Wizara ya Nishati na TANESCO kwa kumtembelea na kujionea ubunifu wake.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga (aliyemwakilisha Kamishna wa Umeme Wizara ya Nishati), Naibu Mkurugenzi Mtendaji – Usafirishaji wa TANESCO, Mha. Isaac Chanji (aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO) na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.

# Kaimu Katibu Mkuu Nishati, akagua eneo la mradi wa umeme wa Ruhudji

## ■ Timu ya Wataalam yaundwa kuanza kazi za awali utekelezaji mradi

**Na Zuena Msuya, Njombe.**

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ameongoza timu ya Wataalam iliyoundwa kutoka Wizara ya Nishati pamoja Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukagua eneo kutakapojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhudji.

Timu hiyo iliundwa mahsusi kwa ajili ya kusimamia kazi za awali kabla ya kuanza rasmi za ujenzi wa mradi huo, ambapo timu hiyo itashirikisha Taasisi na Wizara mbalimbali. Ziara hiyo ilifanyika Januari 12,2021, ikiwa na lengo la kukagua na kuona jiografia ya eneo husika lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe mkoani Njombe.



Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) akiteremka mlima kuelekea eneo la Mto Ruhudji, wakati wa ziara yake na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ya kukagua na kuona jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto huo lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani, Njombe mkoani, Njombe, iliyofanyika Januari 12, 2021.



Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) akisaini Kitabu, wakati wa ziara ya kukagua na kuona jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji, lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 12, 2021.

Kwa mujibu wa Mhandisi Masanja, mradi huo unatarajiwa kuzalisha takribani megawati 358 ambazo zitaingizwa katika gridi ya Taifa pindi mradi huo utakapokamilika.

Kwa mujibu wa mipango ya Serikali, mradi huo utaanza kujengwa mwezi Julai 2021 na utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 36.

Mhandisi Masanja, amewatoa hofu watanzania kuwa, endapo mradi huo

# Kaimu Katibu Mkuu Nishati, akagua eneo la mradi wa umeme wa Ruhudji

utalazimika kuchukua baadhi ya maeneo ya wakazi wanaozunguka eneo la mradi, sheria na taratibu za nchi zitafuata ili kila mmoja apate haki yake ikiwemo kulipwa fidia.

“Mradi huu ni muhimu sana kwetu na umekuja wakati sahihi kwa kuzingatia uchumi wa viwanda, kwani utaongeza kasi ya uwekezaji katika ujenzi viwanda vipya, kuongeza na kuboresha uzalishaji wa katika viwanda vilivyopo sasa, vilevile kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na umeme mwingi, wa uhakika, wa kutosha na wa gharama nafuu nchi nzima.”Alisema Mhandisi Masanja.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka alisema kuwa, Shirika hilo limeupokea mradi huo, na kwamba wako tayari kuanza utekelezaji wa ujenzi wake kulingana na taratibu na miongozo ya Serikali.

Vilevile, alisema kwa kuwa TANESCO ndiyo msimamizi mkuu wa



Meneja Mwandamizi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Salome Mkondela (mbele) na Meneja wa TANESCO mkoani Njombe, Mhandisi Rukia Mpako wakipita katika daraja la muda lililowekwa ili kuwezesha wataalam kukagua sehemu ya eneo la Mto Ruhudji ambalo limegawanyika mara mbili katika eneo moja, wakati wa ziara ya Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO, kukagua na kuona jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto huo, lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 12, 2021.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka, akipita katika daraja la muda lililowekwa ili kuwezesha Wataalam kukagua sehemu ya eneo la Mto Ruhudji wakati wa ziara ya Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ya kukagua na kuona Jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto huo,lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 12, 2021.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka (kulia), Kamishna Msadizi wa Umeme Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga, (wa pili kushoto) wakiwa katika moja ya sehemu ya eneo la Mto Ruhudji wakati wa ziara ya Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO kukagua na kuona Jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto huo, lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 12, 2021.

# Kaimu Katibu Mkuu Nishati, akagua eneo la mradi wa umeme wa Ruhudji



Picha ya Muonekano wa Mto Ruhudji kutoka juu, baada sehemu mbili za mto huo zilizogawanyika, kuungana na kutiririsha maji kuelekea eneo la bondeni. Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) walifanya ziara ya kukagua na kuona Jiografia ya eneo hilo lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, Januari 12, 2021.



Muonekano wa sehemu moja ya eneo la Mto Ruhudji ambalo limegawanyika mara mbili katika eneo moja, utakapojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto huo. Eneo hilo lipo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe.



Baadhi ya Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakipita katika daraja la muda lililowekwa ili kuwezesha wataalam hao kukagua sehemu ya eneo la mto Ruhudji  na kuona jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto huo lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, Januari 12, 2021.



Baadhi ya Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakipandisha mlima kutoka eneo la mto Ruhudji utakapojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya mto huo. Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO, walifanya ziara ya kukagua na kuona jiografia ya eneo hilo lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, Januari 12, 2021.

miradi ya umeme nchini, watahakikisha wanasimamia vyema utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo kuanzia hatua za awali na kuhakikisha kuwa unakamilika kwa wakati uliopangwa.

"TANESCO tunauzoefu katika kutekeleza miradi mikubwa na midogo ya kuzalisha umeme ikiwepo ya Maji, kama vile Mtera, Kidatu, Kihansi na huu mwingine mkubwa kabisa wa Julius Nyerere, niwatoe hofu watanzania kuwa mradi huu, utakamilika kwa wakati, na endapo kuna maeneo ya watu katika eneo la kuzunguka mradi sheria na kanuni za nchi zitafuata ili kila mmoja aweze kupata haki yake." Alisisitiza Dkt. Mwinuka.

# Miundombinu ya umeme Ruhudji na Rumakali kunufaisha kwanza vijiji vya pembezoni

**Na Zuena Msuya Njombe,**

Miundombinu ya umeme itayojengwa ili kutekeleza miradi ya kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhudji na Rumakali itawanufaisha kwanza wakazi wa vijiji vitakavyopitiwa na miundombinu hiyo.

Hayo yameleezwa na Meneja Mwandamizi Uwekezaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Costa Rubagumiya wakati wa ziara ya Timu ya Wataalam iliyoundwa kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO kwa ajili ya kusimamia kazi za awali katika kutekeleza miradi ya kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali uliopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Njombe mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 13,2021.

Mhandisi Rubagumiya alisema kuwa, kabla ya kuanza kutekeleza mradi huo, lazima miundombinu muhimu kama vile umeme, barabara na maji iwepo katika eneo la mradi kwa ajili ya kutekeleza mradi husika.

"Lazima tufikishe umeme katika eneo la mradi, umeme huu utatumika kufanya kazi mbalimbali wakati wa utekelezaji wa mradi huo, kama mnavyofahamu katika ujenzi wa miradi kuna kazi nyingi zinafanyika usiku na mchana, sasa bila kuwa na umeme hatuwezi kufanya kazi hizo kwa ufanisi, vilevile miundombinu ya barabara lazima iwepo ili kuwezasha wahusika



Meneja Msimamizi wa Miradi ya Kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali na Ruhudji, kutoka TANESCO, Toto Zedekia, akitoa maelezo kwa Timu ya wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO iliyokagua eneo hilo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme wa Rumakali uliopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe.





Sehemu ya muonekano wa Mto Rumakali uliopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage wilayani Makete mkoani Njombe unaotarajiwa kutumika kuzalisha takribani megawati 222 za umeme kutokana na maporomoko ya mto huo. Timu ya wataalam iliyoundwa kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ilifanya ziara ya kukagua eneo hilo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme.

# Miundombinu ya umeme Ruhudji na Rumakali kunufaisha kwanza vijiji vya pembezoni

kufika kwa urahisi eneo la mradi pamoja na vifaa vinayohitajika, sasa miundombinu hii itapita katika vijiji mbalimbali hadi kufika eneo la mradi, hivyo vijiji hivyo vyote vitanufaika na miundombinu hiyo."Alisema Mhandisi Rubagumiya

Aidha, Rubagumiya aliwataka wakazi wanaoishi pembenzoni mwa miradi hiyo na hata waliopitiwa na miundombinu ya umeme hadi eneo la mradi, kuhakikisha kuwa, wanalinda miundombinu hiyo na kutoa ushirikiano kwa watakaokuwa wanatekeleza miradi hiyo kwa kuwa itawanufaisha watanzania wote.



Msoma Mita za kima cha maji ya Mto Rumakali, Christon Mahenge, ambaye alianza kufanya kazi hiyo tangu mwaka 1973, akieleza uzoefu wa kazi yake, kwa Timu ya Wataalam iliyoundwa kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati ilipofanya ziara ya kukagua eneo hilo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme lililopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe, Januari 13, 2021.



Timu ya Wataalam iliyoudwa kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakipita pembeni ya Mto Rumakali wakati wa ziara ya kukagua eneo hilo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali uliopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe, iliyofanyika Januari 13,2021.

Mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali utajengwa kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe na unatarajiwa kuzalisha takribani megawati 222 ambazo zitaingizwa katika Gridi ya Taifa pindi mradi huo utakapokamilika.

Aidha, mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji utajengwa kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani na unatarajiwa kuzalisha takribani Megawati 358 ambazo zitaingizwa katika Gridi ya Taifa pindi mradi huo utakapokamilika.

Katika utekelezaji wa mipango ya Serikali, mradi wa umeme wa Rumakali utaanza kujengwa mwezi Julai, 2021 na utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 36.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji - Usafirishaji wa TANESCO Mha. Isaac Chanji (akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO), (wa Pili kutoka kulia). Kushoto ni Kamishna Msaidizi wa Umeme wa Wizara ya Nishati, Mha. Innocent Luoga, mara baada ya kuwasili Kawe jijini Dar-es-salaam kwa lengo la kukutana na Mbunifu wa ufuaji umeme kwa kutumia sumaku.



Vijana waliokuwa wakifanya kazi ya kusafisha njia ili kuwezesha ukaguaji wa eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji, lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, Januari 12, 2021.



Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati walipofanya ziara ya kukagua na kuona jiografia ya eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji, lililopo kati ya Kijiji cha Itipula na Lupembe, wilayani Njombe, mkoani Njombe, Januari 12, 2021.



Picha ya pamoja ya Timu ya wataalam iliyoundwa kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ilipofanya ziara ya kukagua eneo litakalojengwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali, lililopo kati ya Kijiji cha Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe.



Muonekano wa daraja katika Mto Rumakali linalotenganisha Kijiji Madiani na Lumage, wilayani Makete, mkoani Njombe.

# WAZIRI KALEMANI APONGEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KWA KASI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI

## KASI YAKE YAKISIWA KUWA NAMBA MOJA AFRIKA

**Na Dorina G. Makaya, Dodoma**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imempongeza Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani kwa kasi ya kusambaza umeme vijijini ambapo hadi sasa zaidi ya asilimia 80 ya vijiji vyote nchini vimepelekewa huduma ya umeme.



Makamu M/Kiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Seif Khamis Gulamali na Katibu wa kamati hiyo Bi. Felister Mgonja pamoja na wajumbe wa Kamati tajwa hapo juu, wakifuatilia kwa makini maelezo ya Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati Kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara kwenye Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini tarehe 20 Januari, 2021 Bungeni jijini Dodoma. Kulia kwa Waziri Kalemani, ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja.

Pongezi hizo zimetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Seif Khamis Gulamali baada ya Taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara ya Nishati kuwasilishwa kwenye kikao cha Kamati hiyo tarehe 20 Januari, 2021, bungeni jijini Dodoma.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati Kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tarehe 20 Januari, 2021 Bungeni jijini Dodoma. Kulia kwake ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja.

Mhe. Seif Khamis Gulamali amesema kuwa, kasi ya usambazaji umeme vijijini ni kubwa na yawezekana Tanzania ni nchi ya kwanza Afrika katika usambazaji wa umeme vijijini.

Akizungumza kufuatia pongezi hizo, Waziri Kalemani amesema, Wizara ya Nishati itahakikisha vijiji vyote 2200 vilivyobakia ambavyo bado havijaunganishwa na umeme, vitapatiwa huduma hiyo ndani ya miezi 18 kuanzia sasa.

Akijibu swali kuhusu maeneo yenye changamoto ya ukatikaji wa umeme hapa nchini, Waziri Kalemani ameeleza kuwa, kwa upande wa Dodoma , Dar-es-salaam na Mwanza, Wizara ya Nishati kupitia TANESCO imefunga mitambo yenye uwezo wa kutoa umeme wa kutosha hivyo endapo kutatokea kukatika kwa umeme, kutakuwa kumetokana na hitilafu za kiufundi.

Aidha, Waziri Kalemani

amekiri kuwa, kulikuwa na changamoto ya umeme kwa Mkoa wa Ruvuma isipokuwa eneo la Masasi na Tunduru na kueleza kuwa kuna vifaa vya kuboresha nguvu ya umeme ( Automatic Voltage Regulators - AVR ) vinaendelea kufungwa ili kuongeza umeme uwe mkubwa kwa ajili ya watumiaji.
Aliongeza kuwa, ufungaji wa vifaa vya AVR unafanyika pia katika Jimbo la Nyasa na utakuwa umekamilika ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa na hivyo upatikanaji wa umeme katika maeneo husika utaimarika.

Akijibu swali kuhusu ratiba ya utekelezaji wa kazi za Wakandarasi wa umeme katika maeneo yanayopitiwa na miradi ya umeme, Waziri Kalemani amesema, “tumewasihi sana Wakandarasi wanapofika

# WAZIRI KALEMANI APONGEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KWA KASI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI

kwenye maeneo husika, wakutane nanyi Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Wilaya. Kwanza, kutoa taarifa kuwa wameingia kwenye maeneo yenu lakini pia wajue wanaanzia maeneo gani yenye kero ili kushauriana nao mahali pa kuanzia. Tutakapokuwa tunazindua tutawakabidhi kwenu Wakandarasi hao ili mkae nao wajue waanzie wapi.” Amesema Dkt. Kalemani

Akielezea kuhusu upatikanaji wa mafuta kwa maeneo ya vijijini na miji midogo, Dkt. Kalemani ameieleza Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa, Wizara ya Nishati ina mpango wa kuendelea kusambaza vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini na miji midogo kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa nishati ya Mafuta na usalama kwa watumiaji wa maeneo tajwa.

Waziri Kalemani amefafanua kuwa, katika utekelezaji wa suala hilo, kanuni zinapitiwa ili kupunguza gharama za uwekezaji wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini na miji midogo ili kuweza kupata wawekezaji wengi kwenye maeneo hayo.

Ameongeza kuwa, Wizara ya Nishati, inafikiria kujenga vituo rahisi vya pampu moja, ambavyo uwekezaji wake utakuwa nafuu.

Vikao vya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini vilivyoanza jijini Dodoma tarehe 20 Januari, 2021, vinatarajiwa kukamilika tarehe 22 Januari, 2021.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akiwasilisha Taarifa ya Wizara ya Nishati Kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tarehe 20 Januari, 2021 Bungeni jijini Dodoma. Kulia kwake ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja.







# WANANCHI WA KAGERA WATOA KERO ZAO ZA UMEME KWA NAIBU WAZIRI BYABATO

## TANESCO NA REA WAELEKEZWA KUTATUA CHANGAMOTO HIZO

**Na Dorina Makaya – Kagera**

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, amekutana na wananchi wa Mkoa wa Kagera, Uongozi na Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), baadhi ya Watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bukoba, kusikiliza kero za wananchi wa Kagera kuhusu huduma ya umeme.

Miongoni mwa kero zilizotolewa na wananchi hao wa mkoa wa Kagera ni baadhi ya wananchi kufyekewa mazao yao ikiwemo migomba na mazao mengine wakati wa kupitisha miundo mbinu ya umeme, umeme kuwa hafifu wakati wa mahitaji makubwa kuanzia saa Moja jioni hadi saa Tatu usiku katika baadhi ya maeneo ya Bukoba na Bunazi wilayani Misenyi.

Kero nyingine walizotoa ni kuchelewa kulipwa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi wa Kakono utakaozalisha umeme wa megawati 87 katika mto Kagera, kuchelewa kuunganishiwa umeme baada ya kulipia na baadhi ya vijiji kurukwa kuunganishiwa umeme huku vijiji vya mbele vikiwa vimeunganishiwa umeme.

Akijibu kero zilizotolewa na wananchi wa mko huo, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato ameilekeza TANESCO na REA, kutatua changamoto hizo zilizotolewa na wananchi hao na kuhakikisha wateja wote 881 waliolipia huduma



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Kagera, Uongozi na watumishi wa TANESCO, baadhi ya Watumishi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bukoba, mara tu baada ya kusikiliza kero za wananchi wa Mkoa wa Kagera kuhusu huduma ya umeme. (Kushoto kwa Naibu Waziri Byabato), ni Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, na Msimamizi wa Miradi Kanda ya ziwa kutoka Wizara ya Nishati, Mha. Edson Ngabo. kutoka kulia kwa Naibu Waziri Byabato, ni Meneja wa Kanda ya ziwa Mha. Henryfried Byabato na anayefuatia ni Msimamizi wa Miradi Kanda ya ziwa kutoka REA Mha. Ernest Makale.



Mwananchi wa mkoa wa Kagera, kijiji cha Kihanga, wilaya ya Karagwe, Bennie Mushumbuzi, akitoa kero yake kuhusu umeme wakati wa Mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa mkoa Kagera, tarehe 22 Desemba, 2020.

# WANANCHI WA KAGERA WATOA KERO ZAO ZA UMEME KWA NAIBU WAZIRI BYABATO



Wananchi wa Mkoa wa Kagera pamoja na washiriki wengine wa mkutano huo, wakifuatilia kwa makini mkutano wa kutatua kero za huduma ya umeme mkoani Kagera.

ya umeme hadi tarehe 22 Desemba, 2020, wawe wamepatiwa huduma hiyo, ifikapo tarehe 31 Januari, 2021.

Aidha, Naibu Waziri Byabato ameilekeza TANESCO kuhakikisha kuwa, kazi zote zilizoachwa na mkandarasi wa REA II kuwa zinakamilishwa ifikapo mwezi Mei, 2021.

Naibu Waziri Byabato, amewaelekeza TANESCO kuitumia ipasavyo ofisi ya uhusiano kwa wateja na kuhakikisha kwamba wateja wanapatiwa taarifa za hatua mbalimbali za maombi yao kuhusu kuunganishiwa umeme kwa njia ya simu au ujumbe mfupi wa maandishi.

Vilevile, Naibu Waziri wa Nishati, amewaelekeza TANESCO wawajulishe wateja kama kuna matengenezo yoyote ya lazima au hitilafu zinazotokea katika miundombinu ya umeme na kuwaelekeza TANESCO kuwaunganishia umeme wateja ndani ya siku 7 mara baada ya kulipia.

Akizungumzia suala la vitongoji ambavyo bado havijaunganishiwa umeme, amesema kuwa, vitaunganishiwa umeme katika mpango maalum wa kuunganisha umeme wateja kwenye vitongoji vyote nchini ( Densification).

Akijibu kuhusu mazao yaliyokatwa wakati wa kupitisha miundombinu ya umeme, Naibu Waziri Byabato, amesema, Mradi wa REA unaotekelezwa, umegharamiwa na Serikali kwa asilimia 100, hivyo hauna fidia na kuwaomba wananchi kuwa, waruhusu miundombinu hiyo ipite, ili wapatiwe huduma ya umeme.

Akijibu kuhusu fidia ya Mradi wa umeme wa Kakono, Naibu Waziri Byabato, amesema Serikali imekamilisha hatua za uhakiki kwa wale wote watakaoathirika na mradi huo na kuwa, kwa sasa Wizara ya Fedha inashughulikia malipo yao.

Mkutano huo wa kusikiliza na kutatua kero za umeme wanazozipata wananchi wa mkoa wa Kagera, umefanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu mkoa wa Kagera, tarehe 22 Desemba, 2020.

# KAIMU KATIBU MKUU AKAGUA KITUO CHA UMEME GEITA

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja, tarehe 14 Januari, 2021 amekagua kituo cha kupoza umeme cha Mpomvu kilichopo Geita.

Ziara hiyo ni maandalizi ya uzinduzi wa mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita ambao unatarajiwa kuzinduliwa rasmi hivi karibuni na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika ziara hiyo aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka pamoja na watumishi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na TANESCO.



Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika kituo cha kupoza umeme cha Mpomvu kilichopo mkoani Geita. Kushoto ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt. Tito Mwinuka (katikati), Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Uwekezaji kutoka TANESCO, Mha. Khalid James (kulia), Katibu wa Waziri wa Nishati, Robert Dulle, wakiwa kwenye kituo cha kupoza umeme cha Mpomvu kilichopo mkoani Geita.



Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) akiwa pamoja na Kamishna Msaidizi wa umeme Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka pamoja na watumishi mbalimbali wa Wizara ya Nishati, TANESCO na Mkandarasi wa mradi huo.











Picha za matukio mbalimbali katika kituo cha kupoza umeme cha Mpomvu kilichopo mkoani Geita.

# KIKAO CHA NAIBU WAZIRI NA WATENDAJI WA WIZARA YA NISHATI NA TAASISI

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, Januari 13, 2021 amekutana na viongozi wa Idara ya Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati pamoja na Uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika kikao cha kiutendaji kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya mbalimbali kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, akizungumza na viongozi wa Idara ya Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati pamoja na Uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika kikao cha kiutendaji kuhusiana utekelezaji wa miradi mbalimbali kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma, Januari 13, 2021.



Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme, Mha. Styden Rwebangila na Mha. Edson Ngabo, wakiwa kwenye kikao cha kiutendaji kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya mbalimbali, kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma, Januari 13, 2021.









Viongozi mbalimbali wa Idara ya Umeme na Nishati Jadidifu, Wizara ya Nishati, viongozi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wakiwa katika kikao na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, kikao hicho kilifanyika kwenye ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo Mtumba jijini Dodoma.

# WATUMISHI WA WIZARA YA NISHATI WATEMBELEA MRADI WA JNHPP

Watumishi wa Wizara ya Nishati, wamefanya ziara katika Mradi mkubwa wa kufua Umeme kwa maji wa Julius Nyerere(JNHPP) uliopo Rufiji ambao utazalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.

Watumishi hao kutoka kwenye idara na vitengo mbalimbali, licha ya kujionea maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, walipata fursa ya kujifunza kuhusu mradi huo na kupata uelewa zaidi kuhusu faida zitakazopatikana mara baada ya mradi huo kukamilika.













# WANANCHI WAIPONGEZA SERIKALI KWA MAFANIKIO MAKUBWA ILIYOYAPATA KATIKA UGUNDUZI WA RASILIMALI YA GESI ASILIA NCHINI

- **Wafurahia upatikanaji wa nishati ya kupikia kwa bei nafuu na ya uhakika**
- **Waziri Kalemani amuagiza Mkurugenzi TPDC kukamilisha mradi ndani ya miezi 6**
- **Tanzania Inaongoza kwa kuwa na gesi nyingi Afrika Mashariki**

**Na Dorina Makaya – Dar - es - Salaam**

Wakazi wa Mtaa wa Nzasa, Kata ya Kijitonyama, Wilaya ya Kinondoni, wameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi mahiri wa Rais John Joseph Pombe Magufuli kwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Tanzania kutokana na jitahada zake za kuendeleza utafutaji na ugunduzi wa rasilimali Gesi Asilia na mpango mahususi uliopitishwa na Serikali, wa kuwawezesha wananchi wa ngazi zote kiuchumi kupata nishati ya gesi kwa gharama nafuu.

Wakazi hao wa Nzasa, wameelezea furaha yao kuhusiana na mpango huo wa kuunganishiwa mfumo utakaowawezesha kupata nishati ya Gesi Asilia kwa gharama nafuu, ikilinganishwa na nishati nyingine za kupikia, wakati Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alipofanya uzinduzi wa Mradi wa Kuunganisha Gesi asilia majumbani kama nishati ya kupikia, tarehe 23 Januari, 2021
Aidha, wananchi hao, wamemueleza Waziri Kalemani kuwa, wamevutiwa na taarifa hizo za ujio wa nishati hiyo ya Gesi Asilia na ndio maana wamejitokeza kwa wingi katika tukio hilo la uzinduzi wa Mradi huo.

Wamemshukuru Waziri Kalemani, kwa jitihada anazozifanya katika kukuza Sekta ya Nishati nchini na kuomba nishati hiyo ya gesi iunganishwe kwa haraka ili iwafikie wananchi wenye kipato cha chini.

Akijibu kufuatia ombi la wananchi hao, Waziri Kalemani amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Dkt. James Mataragio kuwa, miundombinu ikikamilika, gesi itakayokuwepo katika kituo hicho cha Nzasa, iende pia kwa kaya zote za karibu na kituo hicho.

"Lakini pia gesi hii isiishie hapa Nzasa tu, bali iende kwenye mitaa mingine na uwe ni muendelezo wa maeneo mengine mengi." Amesema Dkt. Kalemani.

Waziri Kalemani amewaelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Wafanyakazi pamoja na Mkandarasi wa mradi huo, waanze kazi ya ujenzi wa miundo mbinu ya gesi eneo la Nzasa mara moja, ili ndani ya mwezi mmoja maendeleo ya kazi hiyo yawe makubwa zaidi.

Aidha, Waziri Kalemani amemuelekeza Dkt. Mataragio, kuhakikisha kazi hiyo ya kujenga miundo mbinu ya Gesi Asilia katika eneo la Nzasa, inakamilika ndani ya miezi sita badala ya mwaka mmoja, kwa kuwa Serikali imetenga fedha na kilichobaki ni suala la kujipanga kwa utekelezaji na wananchi wanasubiria kwa hamu kubwa huduma hiyo.

"Ikifika tarehe Juni 23, mwaka huu, nitakuja kukagua kuangalia iwapo tayari wananchi wa Nzasa wameanza kutumia huduma ya gesi asilia" amesema Dkt. Kalemani.

Dkt. Medard Kalemani, amesema, Serikali imepata mafanikio makubwa kufuatia jitahada zake za kuendeleza utafutaji na ugunduzi wa rasilimali Gesi Asilia hadi kufikia futi trilioni 57.54 mwaka 2021 ikilinganishwa na futi za ujazo wa gesi trilioni 2.7 zilizokuwepo nchini mwaka 2010 na kuwa na ongezeko la futi za Gesi Asilia 54.84 Waziri Kalemani, amebainisha kuwa, hadi sasa, Tanzania inaongoza kwa kuwa na ujazo mwingi wa gesi kwa nchi za Afrika Mashariki.

Dkt. Kalemani amebainisha kuwa, Serikali imefanya mpango mahususi wa gesi iliyogunduliwa hapa nchini kuhakikisha kuwa gesi hiyo, kwanza kabisa inatumika katika kuzalisha umeme wa kutosha, unaotabirika na wa uhakika.

Waziri Kalemani amesema, takriban MW 892.74 za umeme uliopo, unatokana na rasilimali ya Gesi Asilia.

Amesema, kuna jumla ya MW 1602.24 kwa ujumla wake, lakini kati ya hizo zote, zinazotokana na rasilimali ya gesi ni zaidi ya asilimia 60 hivyo mchango wa gesi kwenye kuzalisha umeme mpaka kufikia hapa ni mkubwa ikilinganishwa na rasilimali nyingine.

# WANANCHI WAIPONGEZA SERIKALI KWA MAFANIKIO MAKUBWA ILIYOYAPATA KATIKA UGUNDUZI WA RASILIMALI YA GESI ASILIA NCHINI

Akifafanua kuhusu mgawanyo wa matumizi ya rasilimali ya gesi hapa nchini, Dkt. Kalemani amesema, katika kiasi cha gesi iliyopo hapa nchini, serikali imepanga kutumia kiasi cha gesi futi za ujazo Trilioni 9 kwenye kuzalisha umeme.

Amesema matumizi ya pili ni kutumia rasilimali ya gesi viwandani ili kupunguza mahitaji ya umeme, mkaa na mafuta kwa baadhi ya viwanda vinavyotumia rasilimali hizo.

Waziri Kalemani amesema, hadi sasa viwanda zaidi 48 vimeunganishwa kutumia rasilimali ya gesi na kuwa Serikali imetenga kutumia walau trilioni 3.8 ya gesi iliyogunduliwa hapa nchini kutumiwa viwandani.

Dkt. Kalemani amesema matumizi ya tatu ni katika makazi ya watu na kuwa Serikali imetenga zaidi ya trilioni 1.17 kwa futi zote zilizopo ili iweze kusambazwa na kutumika kwa wananchi kwa matumizi ya majumbani na kuwa uzinduzi wa Mradi wa kuunganisha Gesi Asilia majumbani kama nishati ya kupikia ni kama mwendelezo wake.

Waziri Kalemani ameongeza kuwa, matumizi mengine ni kwenye viwanda vya vyuma ambapo Serikali imetenga jumla ya trilioni 1.1 itakayotumika kwa ajili ya viwanda vya vyuma.




Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa kwanza pichani) akipata maelezo kuhusu namna Mfumo wa Usambazaji Gesi Asilia majumbani utakavyokuwa, kutoka kwa Afisa Utafiti wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Angelindile Marandu wakati wa Uzinduzi wa Mradi huo uliofanyika katika Mtaa wa Nzasa - Sinza, kata ya Kijitonyama jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Jabuari, 2021.

Waziri Kalemani amesema, mgawanyo huo wa matumizi ya rasilimali ya gesi utaendelea kuboreshwa kwa kadri mahitaji yanavyoibuka. Amesema matumizi yote ya gesi iliyopo hapa Tanzania, ikiwemo kuzalisha umeme, matumizi ya viwandani na majumbani, bado Tanzania haijafikia matumizi ya gesi ya ujazo wa trilioni 1. Kati ya Trilioni 57.54 za futi za gesi iliyopo hapa nchini.

Waziri Kalemani amebainisha kuwa hadi sasa matumizi ya gesi hapa nchini ni 0.57 trilioni futi za ujazo. Hivyo inahitajika kuongeza matumizi ya rasilimali ya gesi.

Pia, Waziri Kalemani amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na timu yake kwa kuendelea kusambaza gesi majumbani na maeneo mengine ili itumike sawasawa kwa manufaa ya watanzania. Aidha, Waziri Kalemani amemuagiza Dr. Mataragio kuhakikisha vituo vyote vitano vinavyojengwa vinatumika ipasavyo na kusambaza gesi kwa wananchi.

Vile vile, Waziri Kalemani ameipongeza Serikali ya Wilaya ya Kinondoni kwa kuwa na maeneo mengi yanayopitiwa na mradi wa kuunganishiwa gesi asilia.

Waziri Kalemani amewahamasisha wananchi kutumia rasilimali ya gesi majumbani kwani ni gharama nafuu na ni salama kwa watumiaji.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Dkt. James Mataragio, alisema, kwa kushirikiana na Taasisi za eGA TPDC inaendelea kukamilisha taratibu ili kukamilisha mfumo ambao utamuwezesha mteja wa gesi kwa ajili ya matumizi ya kupikia majumbani kuwa na uwezo wa kununua gesi kwa njia ya simu au benki kama vile inavyofanyika katika umeme. "Gesi asilia ni nishati nafuu na nishati ya uhakika." Amesema Dkt. Mataragio.

Amesema, makadirio ya matumizi kwa familia ya watu sita (6) ni shilingi 29,000 kwa mwezi, ama wastani wa Sh.1,000 kwa siku kwa matumizi ya kupikia vyakula vya aina zote, vikiwemo vile vinavyochukua muda mrefu kupika. Gharama hizi zimekadiriwa kutoka katika takwimu za watumiaji wengi ambao wameanza kutumia gesi

# WANANCHI WAIPONGEZA SERIKALI KWA MAFANIKIO MAKUBWA ILIYOYAPATA KATIKA UGUNDUZI WA RASILIMALI YA GESI ASILIA NCHINI

asilia kwa kupikia tangu mwaka 2015.

Gharama hizi ni nusu ya gharama ya gesi ya mitungi ya LPG yenye ujazo wa kilo 15 kwa mwezi na kuwa gesi hii ni salama zaidi ikilinganisha na nishati nyingine za kupikia kama mafuta ya taa, LPG, kuni, ama mkaa.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa TPDC, amemuahidi Waziri Kalemani kuwa, TPDC itaendelea na juhudi za kusambaza gesi asilia kwa wateja wa majumbani, viwandani, taasisi na pia matumizi ya gesi kama nishati ya kuendeshea magari badala ya mafuta ikiwa ni katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Awali, Dkt. James alimfahamisha Waziri Kalemani kuwa, Mradi anaouzindua unahusisha kuunganisha wateja 506, ambapo wateja 170 wako maeneo ya Sinza na wateja 336 katika maeneo ya Police Barracks-Mgulani.

Aidha, Dkt. Mataragio amesema, mitambo ya kupunguza mgandamizo wa gesi (PRS) iliyofungwa Nzasa na Police Barracks itakuwa na uwezo wa kuhudumia hadi wateja 850 hivyo, idadi ya wateja itaendelea kuongezeka kutoka 506 ya sasa hadi 850.

Amesema, bomba hili la kusambaza gesi asilia katika maeneo ya Sinza litakapokamilika, litakuwa na uwezo



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akikata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua Mradi wa Kuunganisha Gesi Asilia Majumbani kwa ajili ya nishati ya kupikia. Uzinduzi huo umefanyika katika Mtaa wa Nzasa Sinza kata ya Kijitonyama jijini Dar-es- salaam tarehe 23 Januari, 2021. Kulia kwa Waziri Kalemani ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Damas Chongolo na Kushoto kwa Waziri Kalemani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio, anayefuata ni Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta Dkt. Wellington Hudson.

wa kusambaza gesi kwa zaidi ya nyumba 1000. Kwa kuanzia kwa maeneo haya ya Sinza, mradi utaanza kwa kuunganisha wateja 170 wa awali.

Dkt. Mataragio ameweka wazi kuwa, Matumizi ya gesi hii ni rahisi sana ambapo mteja ataunganishiwa gesi asilia na kuwekewa mita maalumu na atanunua gesi kwa njia ya mtandao na kuanza kutumia, huku akifuatilia matumizi yake kupitia mita kama vile ilivyo katika matumizi ya LUKU za umeme.

Amesema, mteja atalipia gesi asilia kwa kadri anavyotumia kwa kununua kiasi cha 'unit' anazohitaji kwa utaratibu unaojulikana kama malipo kabla ya kutumia (pre-paid).

Dkt. Mataragio ameeleza kuwa, gharama hizo ni nusu ya gharama ya gesi ya mitungi ya LPG yenye ujazo wa kilo 15 kwa mwezi na kuwa gesi asilia ni salama zaidi ikilinganishwa na nishati nyingine za kupikia kama mafuta ya taa, LPG, kuni, ama mkaa lakini bado wananchi wanahitajika kufuata maelekezo ya kiusalama katika matumizi ya gesi asilia wakati wote. Dkt. Mataragio amesema, zoezi hili litawafikia wananchi wote na ni endelevu na linakwenda kwa awamu na kuwa litabadilisha maisha ya wananchi kwa kuwa watatumia nishati inayozalishwa hapa nchini ambayo ni nafuu na rafiki wa mazingira.

Amesema, wakati Tanzania ikiwa imeshaingia katika uchumi wa kati, matumizi ya nishati ni kichocheo kikubwa cha maendeleo na ni injini muhimu katika uchocheaji wa kukua kwa uchumi. Amesema, mradi utagharimu fedha za kitanzania takriban Sh. bilioni 2.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Daniel Chongolo, akizungumza katika hafla hiyo alisema, kile wanachozungumza kama serikali na kinachokusudiwa kufanywa na TPDC na timu yake, kiuhalisia, ni mapinduzi makubwa ya kujenga familia moja moja na baadaye kwa nchi nzima kwa ujumla.

Tangu kuanza kwa matumizi ya gesi nchini mwaka 2004 hadi kufikia Juni 2020, fedha za kigeni takribani Dola za Marekani bilioni 14.69 sawa na Shilingi trilioni 34.31 ziliokolewa kwa kutumia gesi badala ya mafuta.

# NAIBU WAZIRI BYABATO AITAKA TANESCO KUPITIA VIGEZO ILI KUIFANYA KIGAMBONI KUWA MKOA WA KITANESCO

**Na Dorina Makaya - Dar-es-Salaam.**

Naibu waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato ameitaka TANESCO kupitia vigezo kuona iwapo Wilaya ya Kigamboni inakidhi vigezo kutangazwa kuwa ofisi ya Mkoa ki-TANESCO na iwapo inakidhi vigezo, wilaya ya Kigamboni itangazwe kuwa mkoa wa ki- TANESCO ili kuendelea kupokea umeme mkubwa na wananchi waweze kuendelea kupata huduma iliyoboreshwa zaidi.

Naibu Waziri Byabato ametoa rai hiyo tarehe 26 Januari, 2021 alipotembelea kituo cha kupoza umeme cha Dege Beach kilichopo wilayani Kigamboni.

Amesema, Wilaya ya Kigamboni ina wateja zaidi ya 30,000, ina mapato zaidi ya bilioni moja kwa mwezi na ni eneo la kimkakati lenye viwanda vya kutosha na bado viwanda vitaendelea kuongezeka hivyo ni lazima changamoto ya umeme itatuliwe.
Naibu Waziri Byabato ameongeza kuwa, Wizara ya Nishati kupitia Shirika lake la TANESCO inaendelea kuzalisha umeme kupitia miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa umeme wa Julius Nyerere ambao utazalisha MW 2115 na unatarajiwa kukamilika tarehe 14/06/2022.

Ameitaja miradi mingine kuwa ni pamoja na Ruhudji, Rumakali, Rusumo na mingine.
Naibu Waziri Byabato ametoa rai kwa wawekezaji, kuwekeza Tanzania kwa kuwa umeme si tatizo tena na kwamba TANESCO itaendelea kusambaza na kuwafikishia umeme wateja.

Akizungumzia kuhusu REA, Naibu waziri Byabato amebainisha kuwa, kwa upande wa REA, kwa sasa kuna mradi wa REA III mzunguko wa pili na ambao utasambaza umeme kwenye vijiji vyote vilivyobakia ambavyo bado vilikuwa havijaunganishwa na umeme.

Naibu Waziri Byabato ameongeza kuwa, kupitia TANESCO Wizara ya Nishati, itaendelea kupeleka huduma kwa wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali ambazo zimekuwepo kwenye eneo la Nishati.
Naibu Waziri Byabato amesema, umeme utakaoletwa kwenye kituo cha Dege beach ni umeme wenye msongo 132kV.

Aidha Naibu Waziri Byabato ameeleza kuwa maendeleo ya ujenzi wa kituo cha Dege beach ni mazuri na umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90. Amesema, kituo hicho kinatarajiwa kukamilika tarehe 28/02/2021 ambapo umeme huo utapelekwa viwandani na majumbani.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato (wa Pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Neema Mushi, Meneja wa Usafirishaji Umeme Makao Makuu ya Tanesco, wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme wa gridi ya taifa kinachojengwa wilayani Kigamboni.

# NAIBU WAZIRI BYABATO AITAKA TANESCO KUPITIA VIGEZO ILI KUIFANYA KIGAMBONI KUWA MKOA WA KITANESCO

Ameongeza kuwa, mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 26 na kwamba kwa sasa Kigamboni itakuwa na uhakika wa kupata umeme wa kutosha na wataalam watahakikisha wanausambaza kwa wananchi.

Naibu Waziri Byabato ameilekeza TANESCO kuhakikisha ifikapo tarehe 28/02/2021, kituo hicho kiwe kimekamilika tayari kwa taratibu za kukizindua na kuwataka wananchi wa Kigamboni pamoja na Watanzania wote kiujumla kuhakikisha wanaendelea kulinda miundombinu ya umeme ambayo nia yake ni kuwafikishia umeme wananchi wote.

Akizungumza kuhusiana na mradi huo wa umeme wa Dege Beach, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Mhe. Sara Msafiri amesema, Mradi huo wa umeme wa Dege beach maarufu kama umeme wa Dege, utasaidia kuondoa changamoto ambazo wananchi wa Kigamboni wamekuwa wakizipata za kukatika kwa umeme mara kwa mara kutokana na chanzo cha umeme huo kutokea mbali Kurasini



Baadhi ya mitambo iliyofungwa katika kituo cha umeme cha Dege wilayani Kigamboni.

na Mbagala na kuwa umeme huo unatembea zaidi ya urefu wa Km 100 kutoka kwenye chanzo cha umeme.

Mkuu wa Wilaya huyo, amesema hali ya kupokea umeme kutoka vituo hivyo unapelekea uwezekano wa kupata athari nyingi, mfano, inapotokea tatizo kwenye vyanzo hivyo vya Kurasini na Mbagala na kulazimika kuzima umeme, Wilaya ya Kigamboni nayo huathirika.

Mhe. Msafiri amesema,ujenzi wa kituo utakapokamilika, kutakuwa na line mbili ambapo moja itakuwa inapeleka umeme Viwandani na nyingine itakuwa inapeleka umeme Majumbani.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato (kushoto) akioneshwa mitambo mbalimbali ya kupoza umeme iliyofungwa kwenye kituo cha Dege, wilayani Kigamboni kikigharimu jumla ya shilingi Bilioni 26.

# WAZIRI KALEMANI ATOA MIEZI 6 KWA MKANDARASI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME LUGURUNI KUKAMILISHA UJENZI

**Na Dorina Makaya, DSM**

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani ametoa miezi 6 kwa Mkandarasi anayejenga kituo kipya cha Kupoza umeme cha Luguruni jijini Dar es Salaam, kukamilisha ujenzi wa kituo hicho.

Waziri Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 28 Januari, 2021 alipofanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho jijini Dar-e-salaam. Waziri Kalemani amebainisha kuwa, Mradi mzima wa kujenga kituo hicho cha kupoza umeme Luguruni utagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 15.2 na kuwa fedha hizo zimetolewa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Waziri Kalemani amefafanua kuwa, ameamua kutembelea kituo hicho ili kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho kutokana na umuhimu wake hasa kitakapokamilika.

“Hapa nchini tunajenga vituo vingi sana vya kufua umeme ama kupoza umeme, tumeshajenga vituo zaidi ya 134 mpaka sasa na tumekamilisha vituo vipya 24 hivi karibuni vikiwemo vya Singida, Rusumo, Nyakanazi na vingine na tunaendelea kujenga vituo vingine vya kupoza umeme zaidi ya 24 vipya ambavyo navyo vitakamilika ndani ya miezi sita hadi minane inayokuja.” Amesema Dkt. Kalemani.

Waziri Kalemani amesema, lengo la kujenga vituo vya kupoza umeme, ni kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa kutosha, wa uhakika na unaotabirika wakati wote.

Waziri Kalemani ameeleza kuwa, kwa Dar-es-salaam peke yake na Pwani, hadi sasa kuna vituo takriban 11 vya kufua na kupoza umeme ambavyo kazi yake ni kuwafikishia wananchi umeme wa uhakika na unaotabirika baada ya kutoka kwenye uzalishaji wake.

Amebainisha kuwa, pamoja na kuwa jiji la Dar es Salaam, lina vituo vya Ubungo I, Ubungo II, Tegeta, Kunduchi, Ilala, Kurasini, Ilala na kuna kituo kinajengwa eneo la Dege, lakini kituo hicho cha Luguruni ni muhimu kwa maeneo ya Dar-es-salaam kwa kuwa kinakwenda kuhudumia maeneo mengi zaidi.

Ameongeza kuwa, katika



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa kwanza kulia) akitoa maelekezo kwa Mkandarasi M/S ( BEIJING) INDUSTRIAL AND COMMERCIAL CO LTD anayejenga kituo cha Kupoza Umeme Luguruni jijini Dar es Salaam, mara alipotembelea kituo hicho kukagua maendeleo ya ujenzi tarehe 28/01/2021.

# WAZIRI KALEMANI ATOA MIEZI 6 KWA MKANDARASI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME LUGURUNI KUKAMILISHA UJENZI

kituo hicho cha Luguruni, laini ya kwanza itapeleka umeme maeneo ya Maili moja mpaka kuelekea Chalinze na Mlandizi na laini ya pili itapeleka umeme maeneo ya Tegeta, kwenye Hospitali ya Mloganzila ambayo ni hospitali ya rufaa.

Waziri Kalemani amebainisha kuwa, Hospitali ya Mloganzila ilikuwa inapata umeme kutoka Ubungo ambapo ni mbali sana na hivyo umeme uliokuwa unafika kwenye hospitali hiyo ulikuwa unafika tayari ukiwa hafifu.

Amesema kituo cha Luguruni pia kitapeleka umeme, Msigani, Kibamba, Kibwegere, Kisarawe, Maili moja na maeneo ya viwanda.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, (wa kwanza kulia) akitoa maelekezo kwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usafirishaji wa TANESCO Mha. Isaac Chanji ( akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO) wakati Waziri Kalemani alipotembelea Mradi wa kujenga Kituo Kipya cha Kupoza Umeme Luguruni jijini Dar es Salaam, tarehe 28 Januari, 2021.

Waziri Kalemani ameongeza kuwa kukamilika kwa kituo cha Luguruni, kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo na kupunguza mzigo wa mashine nyingine za Ubungo, Songas na maeneo mengine mpaka Kinyerezi. "Kwa hiyo wananchi wa maeneo tajwa yatakayopokea umeme kutoka katika kituo hiki wataanza kupata umeme wa kutosha na wa uhakika ndani ya miezi sita kuanzia sasa." Amesisitiza Dkt. Kalemani

Utekelezaji wa mradi huo ulianza tarehe 01 Aprili, 2020 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Septemba, 2021, lakini Dkt. Kalemani amesema kwa kuwa tayari umeme umefika kwenye eneo la ujenzi, amemuagiza Mkandarasi, M/S (BEIJING) INDUSTIAL AND COMMERCIAL CO LTD kukamilisha kazi hiyo ndani ya miezi sita kuanzia tarehe 28/02/2021.

Aidha, waziri kalemani amemtaka Mkandarasi huyo kupeleka wafanyakazi wote wanaotakiwa kufanya kazi mahali hapo ili kuongeza kasi ya ujenzi wa kituo hicho.

Aidha Waziri Kalemani ametaka vifaa vyote vilivyoko bandarini vinavyotakiwa kutoka ili vifanye kazi vitolewe kuwezesha kufanyika kwa kazi hiyo.

Waziri Kalemani ametoa rai kwa wawekezaji na wadau waanze kuandaa miundombinu ya uwekezaji kwani umeme utakaopatikana Luguruni, utakuwa ni umeme mkubwa.

# TANESCO Dodoma yapewa miezi 6, Makao Makuu ya nchi yapate umeme vijiji vyote

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Dodoma kuwa, ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia sasa, Vijiji na maeneo yote ya mkoa huo yawe yamepata umeme, kuunganisha na kuwawashia wateja, atakayeshindwa kutekeleza hilo atakuwa amejifukuza kazi mwenyewe.

Dkt. Kalemani alisema hayo, wakati wa mkutano wake na wafanyakazi wa TANESCO wa Mkoa wa Dodoma, wenye lengo la kufahamiana, kusikiliza changamoto zinazowakabili wafanyakazi hao pamoja na kutoa maelekezo ya kuboresha utendaji kazi wa shirika hilo uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.

Aliwaeleza wafanyakazi hao kuwa, wao ndiyo wenye dhamana na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Mkoa wa Dodoma



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa Mkoa wa Dodoma, (hawapo pichani) wakati wa mkutano wake na wafanyakazi hao uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.



Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Adam Zuberi, (kushoto), Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Nishati, Daniel Machunda (katikati) na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent luoga, (kulia) wakisikiliza swali kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ( hayupo pichani), wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na wafanyakazi shirika hilo wa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.

unapata umeme wa kutosha na wa uhakika katika maeneo yote, kuunganisha na kuwawashia wateja.

Dkt. Kalemani alisisitiza kuwa, mkoa huo kwa sasa una wakazi wengi sana na bado wanaendelea kuongezeka kwa kuwa ni Makao Makuu ya Nchi, umeme mwingi unahitajika katika shughuli mbalimbali, hivyo lazima kila mfanyakazi awe sehemu ya shirika hilo na afanye kazi kwa kasi zaidi, ubunifu mkubwa na kwa usahihi ili kukidhi mahitaji ya umeme na kuboresha zaidi huduma zitolewazo na shirika hilo.

“Sitakubali kupata aibu ya baadhi ya maeneo na Vijiji vya Makao Makuu ya Nchi, kutokuwa na umeme, mkoa huu unazaidi ya Megawati 400 za umeme, lakini matumizi ni Megawati 45 tu kwa sasa, wakati kuna wateja wengi ambao wanahitaji umeme na maeneo mengine bado hayajafikiwa kabisa na huduma hiyo,TANESCO Dodoma fanyeni kazi!”, alisisitiza Dkt. Kalemani.

Hata hivyo alitoa siku 14, kwa shirika hilo mkoani humo kumfikishia taarifa ya namna walivyojipanga katika kusambaza umeme kwa wananchi, kuunganisha wateja wa zamani na kupata wapya, kuzalisha na kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

# TANESCO Dodoma yapewa miezi 6, Makao Makuu ya nchi yapate umeme vijiji vyote

Vile vile alipiga marufuku kwa baadhi ya watumishi wenye tabia ya kuchelewesha majalada ya kazi, kwa kusema kuwa vitendo hivyo vinachelewesha utendaji kazi na kutotimiza malengo kwa wakati.

Alisisitiza kuwa, asilimia kubwa ya utendaji kazi katika ofisi hufanyika kwa mfumo wa maandishi kupitia majalada, endapo mmoja atachelewa au kukwamisha, kazi husika itachelewa na kutotekelezeka kwa muda uliopangwa.
"Ni mwiko na marufuku kukaa na jalada mezani zaidi ya siku moja ofisini, kama huwezi kulifanyia kazi sema au upeleka kwa wanaoweza kulifanyia kazi, tunataka kazi ziende haraka na kwa wakati, ukiona huwezi kufanya kazi kwa kasi hii ninayotaka ni bora uondoke ofisini! Alisema Dkt.Kalemani.

Katika hatua nyingine, Dkt. Kalemani aliiagiza TANESCO, kuangalia upya utaratibu wa kuajiri au kuwapa kazi wafanyakazi wa muda maalum( STE) ambao muda mwingi wanakuwepo maeneo kazi (Site) kufanya kazi za kuchimba mashimo, kusimika nguzo na kuvuta nyaya.





Meza kuu wakiwa wameshikana mikono kuimba wimbo wa wafanyakazi unaosema Mshikamao Daima, wakati wa mkutano Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na wafanyakazi Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa Mkoa wa Dodoma. uliofanyika Januari 22, 2021 mkoani humo.

Aidha alitaka STE wasiokuwa na mikataba wapewe mikataba, wenye sifa ya ajira waajiriwe na wale wasiokuwa na sifa na wamefanya kazi muda mrefu, wapewe mafunzo maalum ili wapate ajira. Pia alitaka shirika hilo kuboresha maslahi wa wafanyakazi hao na kuangalia namna bora ya kuwapa motisha sehemu za kazi waweze kufanya kazi zao kwa furaha, amani na utulivu na kuboresha utendaji kazi wao.

Sambasamba hilo, alitoa miezi miwili kwa wapimaji na watathmini ( Surveyor) pamoja na watoa namba (Control Number) kwa wateja kwa ajili ya kulipia gharama za kuunganishiwa umeme, kubadilika na kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na taaluma zao, na atakayeshindwa kufanya hivyo afukuzwe kazi.

Dkt. Kalemani aliweka wazi kuwa watumishi wa vitengo hivyo wamekuwa wakilalamikiwa kwa kutotekeleza majukumu yao kwa wakati na kuchelewa kutoa huduma kwa wateja.

Aidha aliliagiza shirika hilo kuwapatia pikipiki wafanyakazi wote wa kitengo tathmini na upimaji kurahisisha utendaji kazi wao.

Akizungumzia kitengo cha huduma kwa wateja, Dkt. Kalemani alitaka wahusika kutumia lugha rafiki na zinazofaa kwa wateja, kuweka watoa huduma vijana ili waweze kufanya kazi kwa kasi na haraka zaidi.

"Vitengo hivi vinalalamikiwa sana, wanatakiwa kubadilika, unakuta mteja amejipanga na yupo tayari kupata huduma, lakini mtathimi hafanyi kazi yake, halikadhalika

# TANESCO Dodoma yapewa miezi 6, Makao Makuu ya nchi yapate umeme vijiji vyote





Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Dodoma wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, wakati wa mkutano wake na wafanyakazi hao uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.

na mtoa namba, ukija huduma kwa wateja anatumia lugha ya mbaya, jamani badilikeni la sivyo mtajifukuza kazi wenyewe", alisema Dkt. Kalemani.

Akizungumia zoezi la kuwaunganishia umeme wateja, Dkt. Kalemani alisema wateja wote wanaohitaji umeme waunganishiwe kwa gharama halisi zilizoelekezwa na Serikali, marufuku kwa mteja kulipa zaidi ili apate huduma hiyo kwa haraka na mapema zaidi ya wenzake, kufanya hivyo ni kutoa Rushwa.

Alisema kuwa kuanzia mwezi Februari serikali itaanza kusambaza na kuunganisha umeme kw vijiji vyote nchini vilivyosalia na kazi hiyo itafanyika kwa kipindi cha miezi 18.



Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Wizara ya Nishati, Daniel Machunda (kushoto) na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent luoga, (kulia) wakibadilishana mawazo, wakati wa mkutano Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa Mkoa wa Dodoma uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.



Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Dodoma wakishikana mikono kuimba wimbo wa wafanyakazi unaosema Mshikamao Daima, wakati wa mkutano Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na wafanyakazi hao uliofanyika Januari 22, 2021 mkoni humo.

# WAZIRI KALEMANI AITAKA TANESCO KUZIUNGANISHIA UMEME KATA ZA CHANIKA NA ZINGIZIWA NDANI YA MIEZI 3

**Na Dorina Makaya - Dar-es-Salaam.**

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani ameitaka TANESCO kuhakikisha Inawaunganishia umeme wakazi wa kata za Chanika na Zingiziwa ndani ya miezi mitatu.

Dkt. Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 28 Januari, 2021 akiwa katika ufuatiliaji na ukaguzi wa utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Wizara ya Nishati na kujionea kuhusu utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa.

Waziri Kalemani amekutana na wakazi wa kata hizo za Chanika na Zingiziwa na kusikiliza kero za wananchi hao na kuzitolea maelekezo ikiwemo kuitaka TANESCO kuwaunganishia umeme mara moja wateja waliokuwa wamelipia kuunganishiwa huduma ya umeme huku baadhi yao wakitakiwa kuunganishiwa huduma hiyo ndani ya siku moja, wengine ndani ya siku tatu.



Pichani Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akimsikiliza kwa umakini na kwa unyenyekevu mkubwa Imamu wa Msikiti wa Mtaa wa Zogoali, Imamu Mohamed Ali Libou alipokuwa akieleza kero yake kuhusu upatikanaji wa huduma ya umeme katika msikiti huo.

Vilevile, Waziri Kalemani ameitaka TANESCO kuhakikisha kuwa ifikapo 28 Aprili, 2021 mitaa ya Zogoali, Kidugalo, Zingiziwa, Yongwe, Dondwe, Vikongoro, Chambala, Chanika na Msongola iwe imeshaunganishiwa umeme.

Aidha, baada ya kukutana na wakazi hao, Dkt. Kalemani alipita nyumba kwa nyumba akikagua kujionea nyumba zilizounganishiwa umeme na ambazo zimetandazwa nyaya kwa ajili ya kuunganishiwa umeme na kuhoji kuhusu wateja ambao wametandaza nyaya kwa muda mrefu na kulipia kupatiwa huduma hiyo lakini bado walikuwa hawajapatiwa huduma hiyo.

“ Mkandarasi, nataka kujua ni kwa nini hadi leo mwananchi huyu bado hajaunganishiwa umeme tangia nilipoweka jiwe la msingi la uzinduzi wa Mradi wa kupeleka Umeme katika Vijiji/ Miji (Peri Urban) katika Kata ya Chanika tangia tarehe 03 Mwezi Agosti, 2019. na kuelekeza mara utekelezaji wa Mradi wa kuunganisha umeme katika vijiji hivi, mwananchi huyu awe wa kwanza kuunganishiwa umeme. Sasa, nawapa siku moja, mteja huyu awe amekwisha unganishiwa huduma ya umeme. Amesema Waziri Kalemani.

Baada ya kukagua nyumba kadhaa alipokuwa akirudi kuelekea kwenye mitaa mingine, Waziri Kalemani alishangazwa kuona mafundi wakiwa kwenye nguzo tayari wakifanya kazi ya kumuunganishia mwananchi huyo umeme.

Waziri Kalemani alielezea kushangazwa na nini kilichokuwa

# WAZIRI KALEMANI AITAKA TANESCO KUZIUNGANISHIA UMEME KATA ZA CHANIKA NA ZINGIZIWA NDANI YA MIEZI 3

kikikwamisha mteja huyo kuunganishiwa umeme kwa wakati kama alivyoelekeza tarehe 03 Agosti, 2019 lakini leo mara baada ya yeye kufika kwa mteja huyo, ameunganishiwa umeme ndani ya nusu saa.

Dkt. Kalemani amewataka wananchi hao kutoa taarifa mara moja kuhusiana na watumishi wa TANESCO, REA na Wakandarasi wanaoomba au kudai rushwa ili kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja.

Aidha, Waziri Kalemani amewaahidi wakazi hao wa kata za Chanika na Zingiziwa kuwa, ifikapo tarehe 28 April. 2021 atarudi kukagua kuona iwapo maelekezo yake yametekelezwa.

Hata hivyo, Waziri Kalemani alielezea kutokufurahishwa kwake na hali ya wananchi zaidi ya 4000 waliokuwa wameomba kupatiwa huduma ya umeme katika ofisi hiyo lakini walikuwa bado hawajapimiwa.

Kufuatia changamoto hiyo, Waziri Kalemani amemsimamisha kazi Msimamizi wa kitengo cha upimaji TANESCO Wilaya ya Chanika Fredrick Kilio na kumtaka Meneja waTANESCO Wilaya ya Chanika Mha. Nickson Babu kutekeleza jukumu hilo ambalo



Msikiti wa Zogoali

alishindwa kumsimamia mtumishi wa chini yake kulitekeleza.

Vilevile, Waziri Kalemani ameiagiza TANESCO kutumia ofisi za Serikali zilizopo katika kata ya Chanika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakazi wa kata za Chanika na Zingiziwa wakati wakiendelea na taratibu za ujenzi wa ofisi, hatua ambayo itawaondolea khadhia wananchi wa Kata za Chanika na Zingiziwa kwenda umbali mrefu kupata huduma katika ofisi za TANESCO.

Awali wateja hao wa TANESCO walikuwa wanalazimika kupata huduma za umeme katika ofisi za TANESCO Wilaya ya Kisarawe.

Katika ziara hiyo, Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, Naibu Mkurugenzi wa TANESCO Mha. Isack Chanji, Mameneja wa Wilaya za Chanika na Kisarawe, Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO, REA pamoja na Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa "Peri Urban" katika Wilaya ya Kisarawe Namis Construction Eng. LTD



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akitoa maelekezo kwa Watendaji wa TANESCO na REA wakati alipotembelea Msikiti wa Zogoali. Kushoto kwa Waziri Kalemani ni Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga.



Naibu Waziri Wa Nishati Mheshimiwa Stephen Byabato, akimsikiliza Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga wakati alipotembelea Mradi wa kuzalisha na kupoza umeme Kinyerezi II, tarehe 26 Januari, 2021. Kulia kwa Naibu Waziri Byabato ni Naibu Mkurugenzi wa TANESCO Eng Isack Chanji.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akikagua ujenzi wa miundombinu katika kituo cha kupoza umeme cha Dege jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Wakazi wa Nzasa wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa kuunganisha Gesi Asilia majumbani kwa ajili ya nishati ya kupikia tarehe 23 Januari, 2021 uliofanyika katika mtaa wa Nsasa - Sinza, jijini Dar-es-salaam.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, akiwa na Meneja wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Dege Beach, Mha. Neema Mushi wakati Naibu Waziri Byabato alipokuwa akisoma tarehe ya kutengenezwa mojawapo ya Transfoma iliyopo kituoni hapo mara alipotembelea kituo hicho tarehe 26 Januari, 2021.



Fundi wa umeme wa TANESCO Damary Sirikwa (wa kwanza kushoto) akiwa pamoja na mafundi wenzake wakivuta nyaya kwa ajili ya kuzitandaza katika kituo cha kupoza umeme cha Dege Beach.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*

**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**

Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018

**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*

*Wizara ya Nishati*

*@Nishati2017*

*wizara_ya_nishati_tanzania*

*Wizara ya Nishati*